5. Ni mfano gani hutumika kuonyesha utayari wa Baba kutupea msaada wakati wa uhitaji? Luka 11:11-13.
6. Ni wapi ambapo Bwana alisimama wakati alipokuwa akipitia Samaria? Yohana 4:4-7.

   **Maelezo:** Wakati Mwokozi alipokuwa akielekea Galilaya, maili 100 kaskazini ya Yerusalemu, alisimama katika Samaria katika bonde nzuri linaloelekea mashariki kwenye mto Yordani. Hapa alipata kisima cha Yakobo, ambapo alikuwa amechoka akaketi chini kupumzika. Kulikuwa na uwezekano kwamba alikuwa mdhaifu wa uchovu na kuwa na kiu baada ya safari ndefu.
7. Jinsi gani Mwokozi alianzisha mazungumzo na mwanamke kisimani? Mstari wa 7.
8. Jinsi gani mwanamke alimpokelea, na ni jambo gani lililoonekana kuwa moyoni mwake zaidi? Yohana 4:8, 9.
9. Jinsi gani Yahshua aliyageuza mazungumzo ili kuyafikia mahitaji yake ya kiroho? Yohana 4:10-14.

   **Maelezo:** Huu ni mfano bora kwetu sisi kuufuata. Kwa nyakati zote tunapaswa kuyageuza mazungumzo yetu ili kuwasaidia kiroho na kuwapa mahitaji ya milele ya wale ambao sisi hukutana nao.



14. Wakati huyu mtoto alipotimia umri wa siku nane, walifanya nini kulingana na sheria na yeye aliitwa jina lipi? Luka 2:21 (sehemu ya kwanza).
15. Alipewa jina hilo na nani kabla ya kuchukuliwa mimba? Luka 2:21(Sehemu ya mwisho).
16. Nani alikuwa mfalme wa Yudea wakati huu? Ambaye pia alikuja Yerusalemu? Mathayo 2:1.
17. Maswali yao yalikuwa gani? Ni sababu gani wao walizotoa kwa ajili ya kuja? Mathayo 2:2.

************************************

**Somo la Julai 25, 2026 (Av 11, 5786).**

## MAJARIBU YA YAHSHUA

**Somo Kuu: Mathayo 4**
**Fungu La Kukariri: Mathayo 4:23**

1. Je! Yahshua aliongozwa na nani ili ajaribiwe? Mathayo 4:1
2. Baada ya kufunga siku arobaini, alipata hali gani? Aya ya 2
3. Jaribu lake la kwanza lilikuwa lipi? Aya ya 3
4. Shetani alishindwaje katika jaribu hilo? Aya ya 4
5. Jaribu lililofuata lilikuwa lipi? Aya ya 5-6
6. Shetani alishindwaje tena? Aya ya 7
7. Yahshua aliahidiwa nini ikiwa angemwabudu Shetani? Aya ya 9
8. Silaha ya Masihi ya kushinda jaribu hili ilikuwa nini? Aya ya 10





***"Utakieni Yerusalemu amani; Na wafanikiwe wakupendao" Zaburi 122:6***



# Masomo Ya Bibilia

***kwa***

**KANISA LA ELOHIM (COG)**
**Siku Ya Saba (7th day)**

Robo Ya Tatu
2026

Ya
Julai, Agosti, Septemba.
**(Tamuz, Av, Elul, Tishrei)**

Watenda kazi wanahitajika,
Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache...

**Tuma maombi yote kwa S.L.P 568,**
**Jerusalem — Israel**

9. Baada ya kushindwa kumshinda Yahshua, Shetani alifanya nini? Yahshua alipata msaada gani? Aya ya 11
10. Baada ya kushinda majaribu hayo, Yahshua alifanya nini? Luka 4:14
11. Wakati huo Yohana alikuwa wapi? Mathayo 4:12
12. Yahshua aliweka makao yake wapi? Aya ya 13
13. Ni unabii gani uliotimizwa? Aya ya 14-16
14. Yahshua aliendelea kuhubiri ujumbe gani? Aya ya 17

************************************

**Somo la Agosti 1, 2026 (Av 18, 5786).**

## YAHSHUA ALAANI MAPOKEO YA WANADAMU

**Somo Kuu: Mathayo 15: 1-20.**
**Fungu La Kukariri: Mathayo 15: 9.**

1. Baada ya kulisha makundi, ni nani waliokuja kwa Yahshua? Mathayo 15: 1.
2. Je! Ni mashtaka gani waliyoweka kwa wanafunzi wake? Mathayo 12: 1, 2.
3. Je! Yahshua aliwashutumu kwa nini? Mstari wa 3
4. Yahshua alitoa shutuma hiyo kwa msingi gani? Jinsi gani hii iliwathiri katika kutii amri za Elohim? Mstari wa 4-6.



8. Je! Heshima ya kweli itampataje mwaminifu wa Bwana Elohim wetu? 1 Pet. 5: 1-4.
9. Hata ingawa mwanadamu anaweza kuwa katika cheo cha juu na kustawi, je! Inamruhusu kuwa na kiburi? Zab. 39: 5; 18:27.
10. Je! Uzima wa mtu unahusisha vitu alivyo navyo? Luka 12:15.
11. Je! Nini kitatokea kwamtu aliyeinuliwa na ambaye anajitumainia? Luka 12: 16-21.

************************************

**Somo la Septemba 12, 2026 (Tishrei 1, 5787).**

## MWOKOZI, MFANYAKAZI WA KIBINAFSI

**Somo Kuu: Yohana 4:1-42**
**Fungu La Kukariri: Yohana 4:22, 23.**

1. Ni nani aliyemjia Yahshua usiku? Yohana 3:1, 2.
2. Jinsi gani Yeye alitaja hitaji la nafsi kwa huyo mtawala, na ni haja gani muhimu ambayo yeye alisisitiza? Yohana 3:3-5.
3. Mwenye dhambi anaweza kujipa wokovu wake mwenyewe au yeye anahitaji msaada? Yeremia 13:23; Warumi 8:6-7.
4. Ni kutoka wapi nguvu za kiroho na msaada hupatikana? Luka 11:9, 10.



**Somo la Julai 4, 2026 (Tamuz 19, 5786).**

## MAANDIKO MATAKATIFU

**Somo Kuu: Nehemia 8**
**Fungu La Kukariri: Zaburi 119:105**

1. Biblia yote iliandikwa kwa uwezo wa nani? 2 Timotheo 3:16
2. Je! Ni nani alikuwa wa kwanza kuandika Maandiko Matakatifu? Kutoka 24:12
3. Je! Maandiko hayo yaliandikwa juu ya kitu cha aina gani? Kutoka 31:18; 32:15-16

   **Maelezo**: Kuandikwa kwa Amri za Elohim kwenye mbao mbili za mawe kuna umuhimu katika njia mbili: (1) Jiwe ni mojawapo ya vitu vinavyodumu kwa muda mrefu sana. (2) Sheria ya Elohim, yaani maneno yaliyoandikwa, yataendelea kuwa na nguvu maadamu mbingu na nchi zitadumu (Mathayo 5:18).
4. Je! Ni nani aliyetengeneza mbao za pili za mawe, na ni nani aliyeziandika? Kutoka 34:1-4; Kumbukumbu la Torati 10:1-4
5. Maandiko Matakatifu, kupitia pumzi ya Elohim, yana uwezo wa kufanya nini? 2 Timotheo 3:15-17
6. Je! Paulo alisema Maandiko yaliandikwa kwa ajili ya nani? 1 Wakorintho 10:11



9. Ni sababu gani alitoa kwa hili? Mstari wa 21.
10. Yahshua alisema nini kuhusu matunda ya kila mti aliopanda unapaswa kuzalisha? Mat. 7:17, 19.
11. Je! Ni kundi gani la watu litakubaliwa kuingia katika ufalme wa Bwana? Mstari wa 21.
12. Je, Yahshua aliona lengo kubwa kuwa nini katika kufanya mapenzi ya Baba Yake Mbinguni? Yohana 4:34.
13. Ni nini ilikuwa lengo lake katika kukamilisha kazi Yake? Mstari wa 35.

    **Maelezo**. - Yahshua akiwa mfano wetu, na Roho Mtakatifu mara kwa mara akimhimiza kila mwana wa Elohim kufuata hatua zake, je! Si kweli kwamba kila mtu anapaswa kuwa na hamu ya kumaliza kazi hii kubwa, ambayo bado inaendelea? Tunaweza wote kuwa wajumbe katika kutoa zaka zetu ili kuchapisha ujumbe wa wokovu.

************************************

**Maelezo**. Sabato lazima itunzwe. Hakuna kazi, au biashara ya aina yoyote inaruhusiwa. Lakini ni lazima tufanye mema siku hiyo. Lazima atolewe shimoni, atakapoanguka ndani yake.

*************************************

**Somo la Septemba 5, 2026 (Elul 23, 5786).**

## GHARAMA NA MATOKEO YA KIBURI

**Somo Kuu: Zab. 10.**
**Fungu La Kukariri: Met. 28:25.**

1. Je! Uovu wa wenye kiburi umelezewaje katika Neno Takatifu la Elohim? Isa. 2: 11-13.
2. Kiburi kilileta nini kwa mji wa Moabu? Yer. 49: 13-16.
3. Je! Ni nini chanzo cha majivuno yote? 1 Yohana 2:16.
4. Ni nini kilichoorodheshwa kwanza kati ya vitu saba ambavyo Bwana anachukia? Methali. 6:16, 17.
5. Kiburi kitafanya nini kwa mtu ambaye amejawa nacho? Methali. 16: 5.
6. Kiburi kilimletea nini Nebukadreza? Dani. 5: 18-21.
7. Badala ya kujaribu kujiinua kwenye vyeo vya juu katika maisha haya, tunapaswa kuwa tunafanya nini? Warumi 12:16.



5. Yahshua alitumia jina gani kuwakashifu? Mathayo 15: 7.
6. Isaya alielezeaje kuhusu kundi hili? Mstari wa 8.
7. Yahshua alisema nini kuhusu aina hii ya ibada? Mstari wa 9.
8. Aliwaita nani wamsikilize? Mstari wa 10.
9. Je, Yahshua alisema ni nini humtia mtu unajisi? Mstari wa 11.
10. Ni nani aliyekwazwa na hilo? Mstari wa 12.
11. Mafarisayo hawa walifananisha na nini? Je! Alisema mwisho wao utakuwa ni nini? Mstari wa 14.
12. Je! Ni hamu gani Petro alionyesha? Mstari wa 15.
13. Swali lake lilidhihirisha nini? Mstari wa 16,
14. Jinsi gani Yahshua alielezea? Mstari wa 17, 18.
15. Ni unajisi gani unaotokana na moyo wa mtu? Mstari wa 19, 20.
16. Ingawa Mafarisayo wamekosea katika suala hili, ni utakaso gani mara dufu unapendekezwa na Paulo? 2 Wakorintho 7: 1 (sehemu ya kwanza).
17. Je! Lengo la utakaso huo ni nini? Mstari wa 1 (sehemu ya mwisho).

*************************************



**Somo la Septemba 26, 2026 (Tishrei 15, 5787).**

## MJUMBE MKUU WA ULIMWENGU

**Somo Kuu: Yohana 15: 1-19,**
**Fungu La Kukariri: Yohana 15: 5.**

1. Ni madhumuni gani maalum ya Bwana wetu Yahshua kuja duniani? Luka 19:10:
2. Ni mtazamo gani Yahshua alisema tunapaswa kuwa nao kwa adui zetu? Mat. 5:44.
3. Tunapofanya wema kwa wale wanaotuchukia na kututumia vibaya, hii sio ishara ya uhusiano wetu halisi na Elohim? Sehemu ya mwisho ya aya 44, 45.
4. Ikiwa tunawapenda tu wanaotupenda sisi, je, tunatofautiana na ulimwengu? Mstari wa 47.
5. Je, tunapaswa kushikilia uovu, chuki, au wivu, mioyoni mwetu hata kwa adui zetu wabaya zaidi? Mat. 6.14, 15.
6. Je, Yahshua alingojea hata adui zake wakaja na kumwomba msamaha, kabla ya kuomba na kumwomba Baba Mbinguni kuwasamehe? Luka 23:34.
7. Yahshua alifundisha nini kuhusu kuweka hazina duniani? Mat. 6:19.
8. Wakati Yahshua alikuwa akiishi maisha yake ya mjumbe, na hivyo kuweka hazina mbinguni, aliwaagiza wafuasi wake kuweka hazina zao wapi? Mat. 6:20.



7. Je! Samweli na Daudi walionyeshaje umuhimu wa Neno la Elohim lililoongozwa na Roho? 2 Samweli 22:31; Zaburi 19:7; 12:6-7; 119:140
8. Neno la Elohim lina nguvu gani? Kumbukumbu la Torati 32:1-4; Isaya 55:10-11
9. Je! Elohim analinganisha na nini maneno ya wale wasiolinena Neno Lake la kweli? Yeremia 7:4 (sehemu ya kwanza); Yeremia 29:8-9; 2 Timotheo 2:16-17; Waefeso 5:6

   **Maelezo**: Neno la Elohim ni kama moto (Yeremia 23:29), lakini mafundisho mengine, kama vile desturi za makanisa na kanuni zilizotungwa na wanadamu, ni bure na yanafananishwa na kitu kinachoharibu na kuangamiza. Kwa hiyo, watu wanaposhambulia Neno la Elohim wakidai kwamba halijakamilika, na kutegemea kamusi, ensaiklopidia au vitabu vingine kuthibitisha madai yao, tusidanganywe na mafundisho hayo yasiyo na msingi. Badala yake, na tuendelee kuichukua Biblia Takatifu pekee kama msingi wa imani yetu.
10. Je! Yahshua alisisitizaje umuhimu wa Neno la Elohim? Yohana 12:48; 14:24
11. Je! Neno la Elohim litatufanyia nini tukilitii? Waefeso 5:25-26; Yohana 15:3; 17:17
12. Je! Paulo alisema nini kuhusu jinsi Neno la Elohim litakavyopuuzwa katika siku za mwisho? 2 Timotheo 4:1-4; Tito 1:9-14

**Somo la Agosti 8, 2026 (Av 25, 5786).**

## KUZAMISHWA (NDANI YA MAJI), NJIA YA ELOHIM YA UBATIZO

**Somo Kuu: Mathayo 3.**
**Fungu La Kukariri: Wakolosai 2:12**

1. Ubatizo wa Yahshua, jinsi gani ulifanywa na ulifanywa na nani? Mathayo 3: 13-16.
2. Mtume Paulo anasema nini kuhusu aina ya ubatizo katika siku alizoishi? Wakolosai 2:12.
3. Baada ya Pauli na Sila kufunguliwa kwa miujiza kutoka gerezani, ni mtu gani muhimu na familia waliamini na kubatizwa? Matendo 16: 29-33.
4. Tunapaswa kuenendaje baada ya kubatizwa, au kuzikwa pamoja Naye katika ubatizo? Warumi 6: 4.
5. Tutamvaa aje Masihi? Wagalatia 3:27.
6. Je! Sisi ni kwa kuzamishwa katika maji tumebatizwa katika kifo cha Masihi? Warumi 6: 3-4.
7. Kwa nani, na kwa namna gani, towashi aliyeamini alibatizwa? Matendo 8:38.
8. Ni aina ngapi za ubatizo zilizopo? Waefeso 4: 5.
9. Je, kulikuwa na watu wengi walioamini na kubatizwa baada ya kusikia mahubiri ya Petro siku ya Pentekoste? Matendo 2:41.
10. Je, kulikuwa na wengine ambao waliamini na kubatizwa baada ya kusikia mahubiri ya Filipo



6. Ni mpaka lini na ni kwa muda gani siku ya Sabato inapaswa kutunzwa? Kut. 31:16, 17; Neh. 13:19.
7. Ni rekodi gani inathibitisha kwamba mazoezi haya yalifuatwa wakati Masihi alikuwa anaishi hapa duniani? Marko 1: 21-34.
8. Je, Mwokozi wetu alifanya nini siku ya Sabato? Luka 4:16; Marko 1:21.
9. Je! Ni amri gani ya jumla ambayo Elohim alitupa kupitia nabii, juu ya jinsi tutakavyotumia Sabato? Isa. 58, 13, 14.
10. Mbali na kuhudhuria mikutano ya kidini siku ya Sabato, ni nini kinaruhusiwa? Mat. 12: 10-13.
11. Tufanye nini na kazi zetu siku ya Sabato? Luka 13:15, 14: 5.
12. Je! Maandiko yanasema nini juu ya haki ya kufanya kazi siku ya Sabato? Ikiwa kwa hivyo tunaweza kuokoa mazao yetu wakati wa mavuno, je! Tunapaswa kuyaona yameharibika vinginevyo? Kut. 34:21, 35: 2.
13. Ni nini imesemwa kuhusu kuenda safari ndefu siku ya Sabato? Mat. 24: 15-20.
14. Kupika na kuoka kwetu kutafanywa lini, Ijumaa au Sabato? Kut. 16:11, 23.
15. Ni vipi kuhusu kwenda dukani siku ya Sabato? Kut. 16: 27-29.
16. Je! Elohim kupitia Yeremia alisema nini juu ya kubeba mizigo siku ya Sabato? Yer. 17:21, 22.
17. Je! Biblia inasema nini juu ya biashara siku hii? Neh. 13: 15-22.



13. Je, kuna njia yoyote ya kuokoka kwa wale wanaokataa kulitii Neno la Elohim? Waebrania 2:1-3.

************************************

**Somo la Julai 11, 2026 (Tamuz 26, 5786).**

## KIZAZI NA KUZALIWA KWA YAHSHUA

**Somo Kuu: Mathayo 1.**
**Fungu La Kukariri: Mathayo 1:23.**

1. Je! Mwanzo wa Mathayo umepangwaje? Je! Yahshua anasemekana ni mwana wa nani? Mathayo 1: 1.
2. Je, Luka anasema nini juu ya hili? Luka 1: 30-33.
3. Ni nani alikuwa wa mwisho katika kizazi cha Masihi kutajwa? Mathayo 1:16.
4. Kuna vizazi vingapi kutoka kwa Ibrahimu hadi Daudi; kutoka Daudi hadi utumwani Babeli, na kutoka huko hadi Masihi? Mstari wa 17.
5. Je! Kulikuwa na uhusiano gani kati ya Yusufu na Mariamu kabla ya kuzaliwa kwa Yahshua? Mstari wa 18.
6. Tabia ya Yusufu ilikuwa gani? Alikusudia kufanya nini kwenye hafla hii? Mstari wa 19.
7. Alizuiliwaje kutekeleza mpango wake? Alihakikishiwa nini? Mstari wa 20.



**Maelezo**. - Kwa hiyo ni muhimu sana kuishi karibu na Bwana katika sala ili kuhakikisha kutoa zaka ambapo zitakuwa na faida kwa Yeye na sababu halisi ambayo Bwana Yahshua alikufa. Kuna wadanganyifu wengi na walimu wa uongo ambao hatungependa kusaidia. Mat. 24:24; 2 Tim. 3:13.

9. Ni mifano gani bora katika Agano la Kale kuhusu kutoa fungu la kumi? Mwanzo 14: 18-20; Mwanzo 28: 20-22.
10. Je, Masihi aliidhinisha utoaji wa zaka? Mat. 23:23; 22: 15-21.
11. Je, kutoa sadaka pia inahitajika kwetu? Mal. 3: 8, sehemu ya mwisho.

**Maelezo**. — Hatumpi Bwana kitu chochote katika kulipa zaka, kwa kuwa sehemu ya kumi ya mapato yetu ni yake. Anasema ni mali yake. Aliumba mbingu na ardhi. Dunia na vyote vilivyomo ni mali Yake. Angalia Zaburi 24: 1 na 50:10. Anasisitiza na kuimarisha. Heb. 1: 3.

Zaka iliyo takatifu kwa Bwana hutuwezesha kushiriki katika kueneza Injili ya wokovu, kama Mwokozi wetu angefanya kama angalikuwa bado hapa duniani katika mwili. Hivyo hutupa sehemu katika kuhubiri ujumbe wa wokovu kwa ulimwengu wote.

************************************

6. Yakobo hutukuzaje sheria hii? Yakobo 2: 8-9.
7. Tunawezaje kusimama mbele ya Elohim ikiwa tutakaidi sheria hii? Mstari wa 10.
8. Ni kwa njia ipi Yakobo anashawishi mawazo yetu juu ya suala hili? Mstari wa 11.
9. Badala ya kutangua sheria hii, Yahshua anaitukuzaje? Mathayo. 5:27, 28; Isa. 42:21.
10. Yohana anaitukuzaje sheria hiyo? Yohana 3:16 18.
11. Kwa sababu ya nia ya mwili, Kanisa la Elohim litateseka kwa nini siku za mwisho? Warumi 8: 7; Ufu. 12:17.

*************************************

**Somo la Agosti 29, 2026 (Elul 16, 5786).**

## JINSI YA KUTUNZA SIKU YA SABATO

**Maandiko; kusoma: Isa. sura ya 58.**
**Fungu La Kukariri: Luka 14: 5.**

1. Sabato ya kwanza ilitunzwa lini, na nani? Mwa. 2: 1-3.
2. Ni nini kilichoamriwa kuhusu siku ya Sabato? Kut. 20: 8-11.
3. Siku inaanza lini? Mwa. 1: 5.
4. Je! Tuna uthibitisho gani wa Agano Jipya, kwamba siku hujumuisha giza na nuru? Marko 14:30.
5. Jioni, au siku mpya huanza lini? Walawi. 23:32.



juu ya ufalme wa Elohim na Yahshua Masihi? Matendo 8:12.

11. Kwa nini Yohana alibatiza huko Aenoni? Yohana 3:23.

**Maelezo**. Aya zilizo hapo juu zinathibitisha ukweli kwamba kuzamishwa ni njia sahihi ya ubatizo. Ikiwa kunyunyizia mtu maji hutosha, kwa nini Yohana alitaka maji mengi ya kubatiza? Kunyunyizia mtu maji ni makosa, na ni hali ya kusikitisha sana ambayo wengi wamewadanganywa na mafundisho hayo na bado wanataka kuyashikilia. Hebu tuombe ili waweze kuona mwanga wa kweli na kukubali nuru ya kweli na kukubali mpango wa Elohim wa wokovu kwa ukamilifu wake.

*************************************

**Somo la Agosti 15, 2026 (Elul 2, 5786).**

## MVUA YA ZAMANI

**Somo Kuu: Yoeli 2: 12-32**
**Fungu La Kukariri: Yoeli 2:23**

1. Ni kupitia chanzo gani cha asili ambacho Baba yetu wa Mbinguni husababisha nchi kufanikiwa? Walawi. 26: 4,5
2. Alitajaje chanzo cha baraka hii ya asili? Kumbukumbu 28:12, Malaki 3:10 sehemu ya mwisho



**Somo la Septemba 19, 2026 (Tishrei 8, 5787).**

## KUISHI KWA AJILI YA YAHSHUA NA KUWA MWAMINIFU KATIKA UWAKILI

**Somo Kuu: Mathayo 25: 14-30.**
**Fungu La Kukariri: Yohana 15: 2.**

1. Je! Sababu ya Masihi ilikuwa gani kuja duniani? Luka 19:10.
2. Je! Petro alisema nini juu ya kazi ya Bwana? 1 Petro 2:21.
3. Ni kwa maneno gani ya upendo tunaambiwa tufuate mfano Wake? Mat. 16: 24-26.
4. Je, kuna thawabu kubwa kwa kuwa wakili mwaminifu? V. 27.

   **Maelezo**. - Kuna njia nyingine za kutoa maisha yetu badala kuipeana katika kifo kama shahidi. Mtu anaweza pia kupoteza maisha yake katika huduma kwa Bwana Yahshua Masihi.

5. Ni nini maana katika Biblia kuhusu fungu la kumi? Walawi. 27: 30-32.
6. Fungu la kumi ni la nani? Mstari wa 30.
7. Machoni pa Bwana tunaonekana aje ikiwa tutashindwa kulipa kile kinachomstahili? Mal. 3: 8.
8. Ni adhabu gani ya kutisha ambayo itamjia mtumishi asiye na manufaa? Mat. 25:30.



8. Je! Malaika alisema Mariamu atamzaa nani? Mstari wa 21.
9. Je! Hii yote ilikuwa kulingana na nini? Mstari wa 22.
10. Je! Isaya alitabiri nini juu ya hili? Mstari wa 23.
11. Je! Paulo anasema nini kuhusu utimilifu huu? 1Timotheo 3:16.
12. Je! Yusufu alikuwa na mtazamo gani baada ya ndoto hii? Mathayo 1:24.
13. Je! Mtoto Masihi alipewa jina gani? Mstari wa 25.
14. Umuhimu wa jina hili umesisitizwa vipi? Matendo 4: 10-12; Wafilipi 2: 9-11.

*************************************

**Somo la Julai 18, 2026 (Av 4, 5786).**

## KUZALIWA KWA YAHSHUA

Maandiko matakatifu yanatueleza kwamba Masihi ni wa "nyota ya Yakobo" (Hesabu 24:17); "Nyota ya siku" (2 Petro 1:19); "Nyota yenye kung'aa ya asubuhi" (Ufunuo 22:16). Mamajusi kutoka Mashariki walikuwa si wataalamu wa nyota tu, kama baadhi ya watu ufundisha. Waliona "Nyota" na wakaamua "kuja kumwabudu." Tunaamini walikuja kwa kuongozwa na Elohim, "kwa maana dunia kwa hekima haikumjua Elohim.", 1 Wakorintho 1:21.

3. Waisraeli walihitaji nini wakati wa mvua ulipofika? Zakaria: 10: 1,
4. Je, hali ya ardhi ilikuwa ipi wakati Bwana mwema alizuia mvua? Yoeli 1:12, 17, 18
5. Ni katika hali gani Waisraeli walifurahi tena? Yoeli 2:23, 24
6. Chini ya mvua hii ni nini kingerejeshwa? Mstari wa 25 - 27

   **Maelezo** - Ni dhahiri kutokana na mambo yaliyotangulia na mengine ya vitendo ambavyo bila mvua hakutakuwa na mimea; matokeo ya asili yatakuwa njaa kwa wanadamu na wanyama. Vivyo hivyo ndivyo ilivyo kwetu bila Roho Mtakatifu.
7. Baba wa Mbinguni hutumia mvua ya asili ili kuashiria nini? Hosea 6: 1-3

   **Maelezo**: - Hapo Bwana mwema hutaja baraka za kiroho kama mvua ya zamani na ya baadaye.
8. Ni ahadi gani nyingine iliyofanywa katika mfano huu? Yoeli 2: 28-29
9. Je! Ahadi hii ya mfano ilitimizwa lini? Matendo 2: 1-4.
10. Tunajuaje kwamba tafsiri yetu ni sahihi? Mstari wa 14-17
11. Ni sababu gani Petro aliyotoa kuhusu sababu ya Masihi kutoa udhihirisho huu? Mstari wa 32, 33.
12. Mahubiri haya yaliwaathiri aje? Ombi lao lilikuwa lipi? Mstari wa 37.

************************************



**Somo la Agosti 22, 2026 (Elul 9, 5786).**

## SHERIA TAKATIFU

**Somo Kuu: Warumi 13.**
**Fungu La Kukariri: Warumi 13: 8.**

1. Biblia inasema dhambi ni nini? 1 Yohana 3: 4; Warumi 3:20.
2. Ibrahimu alikuwa na uhusiano gani na Sheria Takatifu ya Elohim? Mwanzo 26: 4, 5.
3. Kitukuu cha Ibrahimu alikataa kufanya nini alipojaribiwa? Mwanzo 39: 7-9.

   **Maelezo**. — Hatuna kumbukumbu kwa undani ya wakati ambapo Elohim alimpa Ibrahimu sheria hizi zote, amri na hukumu na kadhalika. Bali kwa kuwa alizitunza ni ushahidi tosha kwamba alikabidhiwa hizo sheria. Huu ni ushahidi kamili kwamba sheria ilikuwapo kabla ya kupeanwa huko Sinai.
4. Nini maneno gani mengine yanaonyesha kuwa sheria ilikuwapo kabla ya Sinai? Kutoka. 16: 4, 22, 23.

   Maelezo. Hapa tunaona kwamba kwa kukataa kutunza siku ya sabato waliiasi sheria. Huwezi kuondoa sabato kutoka kwa amri kumi.
5. Tunajuaje kwamba hii ndiyo sheria, ambayo huonyesha dhambi? Warumi 13: 8-10.



**Somo Kuu: Mathayo 1:18-25.**
**Mistari ya kumbukumbu: Luka 2:13, 14.**

1. Lengo la safari ya Joseph na Maria kwenda Bethlehemu lilikuwa lipi? Luka 2:1-5.
2. Wakiwa huko Bethlehemu, ni tukio gani la ajabu lilitokea? Luka 2:6, 7.
3. Ni nini kilichosemwa juu ya wachungaji wakati huu? Luka 2:8.
4. Ni utukufu gani wao waliruhusiwa kutazama? Luka 2:9.
5. Ni ujumbe gani wa ajabu malaika waliwapa? Luka 2:10, 11.
6. Ni ishara gani walipewa kuhusu mtoto huyu? Luka 2:12.
7. Ni habari nyingine zipi za utukufu walizopokea wachungaji? Luka 2:13, 14.
8. Wakati malaika waliondoka, ni nini wachungaji waliamua kufanya? Luka 2:15.
9. Wakati walifika mahali paliponenwa na malaika, waliona nini? Luka 2:16.
10. Wachungaji walifanya nini kuhusu habari njema waliopokea? Luka 2:17.
11. Jinsi gani wasikilizaji waliichukua ripoti hiyo? Luka 2:18.
12. Mtazamo wa Maria kuhusu tukio hili ulikuwa upi? Luka 2:19.
13. Jinsi gani wachungaji walidhihirisha furaha yao kwa ajili ya Mwokozi? Luka 2:20.



10. Jinsi gani Yahshua alithibitisha kwa mwanamke huyu kwamba alikuwa tofauti na mtu wa kawaida? Yohana 4:16-18.

    **Maelezo:** Ingawa sisi hatuna uwezo wa kuwaambia watu kuhusu maisha yao wenyewe kama Masihi alivyokuwa, tunaweza kuwaambia kuhusu hali ya ulimwengu; Hali ambayo kwa kimiujiza hutimiza maneno ya manabii wa kale.
11. Yahshua alisema nini kwa mwanamke huyu kuhusu wokovu? Jinsi gani yeye alieleza kuhusu ibada ambayo hukubalika? Yohana 4:22-24.
12. Je, huyo mwanamke alisema nini kuhusu Masihi? Yahshua alifanya tangazo gani? Yohana 4:25, 26.
13. Wakati wanafunzi wa Masihi, ambao walikuwa wameendea chakula, waliporudi kwenye eneo la tukio na kumpa chakula, jibu lake lilikuwa lipi? Yohana 4:31-34.

14. Mwanamke huyo alifanya nini na nini ilikuwa matokeo ya ushuhudiaji binafsi wa Mwokozi? Je, huu ni mfano kwetu? Yohana 4:25-30; 35-42.

************************************